JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2023

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2023

# 021 KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

YALIYOMO ............ iii

DIBAJI ............ iv

1.0 UTANGULIZI ............ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI ............ 2

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA ............ 2
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua ............ 2
2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha ............ 14
2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ............ 17
2.2.1 Swali la 3: Ufahamu ............ 17
2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno ............ 24
2.2.3 Swali la 5: Aina za Maneno ............ 27
2.2.4 Swali la 6: Mawasiliano ............ 30
2.2.5 Swali la 7: Matumizi ya Lugha ............ 34
2.2.6 Swali la 8: Fasihi Simulizi ............ 37
2.2.7 Swali la 9: Fasihi Simulizi ............ 40
2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU ............ 44
2.3.1 Swali la 10: Uandishi wa Barua ............ 44

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA ............ 48

4.0 HITIMISHO ............ 48

5.0 MAPENDEKEZO ............ 50

KIAMBATISHO CHA PEKEE: Uchambuzi wa Viwango vya Ufaulu wa Wanafunzi katika Mada kwa Mwaka 2023 ............ 51

## DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili Mwaka 2023 kwa somo la Kiswahili imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau mbalimbali wa elimu. Taarifa hii inalenga kutathmini muhtasari wa Kidato cha Kwanza na cha Pili ili kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu hususani katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Majibu ya wanafunzi ni kiashiria dhahiri iwapo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa wanafunzi maarifa stahiki katika elimu ya sekondari kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Pili.

Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa Upimaji wa Kidato cha Pili Mwaka 2023 kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 660,969 sawa na asilimia 95.19 walifaulu. Ufaulu huu ulikuwa wa chini kwa asilimia 0.47 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo asilimia 95.66 walifaulu. Sababu zilizowafanya wanafunzi wengi kufaulu vizuri au kwa kiwango cha wastani ni pamoja na kuwa na uelewa wa mada zilizopimwa, kuelewa matakwa ya swali, na kujieleza kwa kutumia lugha fasaha ya Kiswahili.

Aidha, sababu zilizowafanya wanafunzi wachache (4.81%) kupata alama hafifu ni pamoja na kutoelewa matakwa ya swali, kukosa uelewa wa kutosha katika mada nyingi zilizopimwa na uwezo mdogo wa kujieleza kwa lugha fasaha na kutoelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili.

Taarifa hii itawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu mwafaka katika kuboresha elimu kwa ujumla na hivyo kuongeza ufaulu katika upimaji ujao unaoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wachambuzi wa data na wote walioshiriki katika mchakato wa uandishi wa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Somo la Kiswahili kwa Kidato cha Pili uliofanyika mwezi Novemba mwaka 2023 ulikuwa na maswali kumi (10). Maswali hayo yaligawanyika katika sehemu A, B na C ambapo sehemu A ilihusu maswali ya kuchagua na kuoanisha; sehemu B maswali ya majibu mafupi, na C swali la insha. Mada zilizotahiniwa katika sehemu zote zilihusisha *Sarufi*, *Ufahamu*, *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*, *Fasihi*, na *Uandishi*. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu umezingatia kikamilifu muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha Kwanza na cha Pili.

Taarifa hii inachambua viwango vya ufaulu wa wanafunzi wa Kidato cha Pili katika Upimaji wa Somo la Kiswahili Mwaka 2023. Jumla ya wanafunzi 759,791 walisajiliwa kufanya upimaji ambapo wanafunzi 695,269 sawa na asilimia 91.51 walifanya upimaji wa somo la Kiswahili. Kati yao, wavulana walikuwa 318,443 sawa na asilimia 45.80 na wasichana 376,826 sawa na asilimia 54.20. Ufaulu wa wanafunzi katika upimaji huu kwa ujumla ulikuwa mzuri kwani wanafunzi 660,969 sawa na asilimia 95.19 ya waliofanya upimaji huu walifaulu kwa kupata madaraja A hadi D. Kiwango hicho cha ufaulu ni cha chini kwa asilimia 0.47 kikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo, asilimia 95.66 ya wanafunzi walifaulu kwa kupata madaraja A hadi D. Ulinganifu wa ufaulu wa wanafunzi kwa kila daraja kwa mwaka 2022 na 2023 umeoneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Wanafunzi kwa kila Daraja**

| **Mwaka** | **Waliofanya** | **Madaraja** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **A** | **B** | **C** | **D** | **F** |
| 2022 | 634,843 | 78,986 | 107,914 | 289,808 | 129,059 | 27,486 |
| 2023 | 695,269 | 29,428 | 69,074 | 346,946 | 215,521 | 33,431 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa, kiwango cha ubora wa ufaulu kimepungua kwa mwaka 2023 kwani wanafunzi wengi walifaulu kwa kupata daraja C na D. Uchambuzi wa ufaulu unaonesha kuwa ufaulu wa madaraja ya juu A na B ulipungua jambo linaloashiria kushuka kwa ufaulu kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022.

Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya ufaulu, ambavyo ni kiwango *kizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri cha ufaulu kimeanzia alama 65 hadi 100, kiwango cha wastani kmeanzia alama 30 hadi 64, na kiwango hafifu kimeanzia alama 0 hadi 29. Chati mbalimbali zimetumika kufafanua viwango hivyo. Aidha, rangi mbalimbali zimetumika kuwakilisha viwango vya ufaulu. Rangi ya kijani imewakilisha kiwango kizuri, rangi ya njano imewakilisha kiwango cha wastani na rangi nyekundu imewakilisha kiwango hafifu cha ufaulu. Vilevile, sampuli za majibu sahihi na yasiyo sahihi kutoka kwa wanafunzi zimeambatishwa ili kudhihirisha majibu halisi ya wanafunzi.

Kwa jumla, uchambuzi huu unalenga kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi, na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuendelea kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili.

# 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya uchambuzi wa kina wa majibu ya kila swali yaliyotolewa na wanafunzi kwa kuonesha maswali yaliyojibiwa vizuri na yale yaliyojibiwa vibaya. Aidha, sababu za ufaulu wa viwango mbalimbali zimeelezwa bayana kwa kila swali. Vilevile, sampuli za majibu ya wanafunzi kwa kila swali zimeambatishwa ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa katika uchambuzi huu.

## 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) ambapo swali la 1 lilikuwa la kuchagua na lilikuwa na vipengele kumi (10), na swali la 2 lilikuwa la kuoanisha maana na tanzu za fasihi simulizi katika orodha A na B. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 15.

### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua

Swali lilitoka katika mada za *Fasihi Simulizi, Aina za Maneno, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali, Mawasiliano, Uundaji wa Maneno,* na *Uandishi*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukumbuka dhana mbalimbali zinazohusu mada anuai za somo la Kiswahili. Swali lilimtaka mwanafunzi kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo manne (A –

D) kwa kila kipengele. Kila kipengele kilikuwa na alama moja na kufanya swali hili kuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 695,263 sawa na asilimia 99.99 ya waliofanya upimaji katika somo hili. Hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na wanafunzi wengi, ambapo asilimia 95.78 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 1***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 269,469 (38.76%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 7 hadi 10, wanafunzi 396,450 (57.02%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wanafunzi 29,344 (4.22%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata 0 hadi alama 2.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, zaidi ya nusu (57.02%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya dhana mbalimbali zilizopimwa katika vipengele vya swali hili. Aidha, baadhi walionesha kukosa uelewa wa dhana mbalimbali zilizopimwa katika vipengele hivyo. Wanafunzi hao waliweza kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele 3 – 6 na kupata alama za wastani.

Uchambuzi wa kina wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 269,469 sawa na asilimia 38.76 walijibu vizuri swali hili

kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa dhana zilizopimwa. Wanafunzi hao walijibu kwa usahihi vipengele 7 hadi 10 vya swali hili. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama zote.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

   (i) Ni methali ipi inayofanana na methali inayosema, "Mtaka cha uvunguni sharti ainame"?
   A Ujanja mwingi mbele giza.
   B Mjumbe hauawi.
   C Akili nyingi huondoa maarifa.
   D Atangae sana na jua hujua.

   [D]

   (ii) Bainisha ubora wa kuhifadhi kazi za fasihi kwa kutumia njia ya picha na vinasa sauti.
   A Fanani na hadhira huonana ana kwa ana.
   B Wasanii huonekana dhahiri.
   C Huwa na gharama ya kumiliki.
   D Huweza kupotea na kutopatikana tena.

   [B]

   (iii) Mwalimu aliwaagiza wanafunzi wawili wajibizane kishairi mbele ya wenzao darasani. Ni kipera kipi kinawakilisha walichofanya wanafunzi hao?
   A Ngonjera B Majigambo
   C Kichekesho D Igizo

   [A]

   (iv) Sentensi ipi kati ya zifuatazo imeundwa kwa kitenzi kishirikishi?
   A Tanzania ilikuwa inapendeza toka zamani.
   B Watoto wanalima shamba dogo sana.
   C Watu wa mjini si wengi kama wa vijijini.
   D Mto mdogo umejaa majani mengi.

   [C]

   (v) Sauti ya lugha inayotamkwa bila kuwapo na kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa huitwaje?
   A Silabu B Irabu
   C Konsonanti D Mkazo

   [B]

   (vi) Mojawapo ya alama za uandishi ni nukta. Kazi ya alama hiyo ni ipi katika sentensi?
   A Kukariri au kurudia maneno yaliyosemwa.
   B Kuonesha sentensi imefikia mwisho na imekamilika.
   C Kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume.
   D Kuashiria maneno yaliyo kwenye orodha.

   [B]

(vii) Mwalimu aliwataka wanafunzi kuchambua neno "**anacheza**" na kuonesha viambishi vyake. Uchambuzi upi unaonesha mpangalio sahihi wa viambishi?

A Kiambishi awali ni ***a***-, -***na***- na kiambishi tamati ni –***a***
B Kiambishi awali ni –**a** na kiambishi tamati ni –**na**-
C Kiambishi awali ni –**na**- na tamati ni **a**-
D Kiambishi awali ni –***na***- na – ***chez*** – na tamati ni ***a***-

A

(viii) Kisawe cha neno "jokofu" ni kipi kati ya hivi?

A Jiko B Tanuru
C Friji D Stovu

C

(ix) Aina ipi ya kamusi hutumia lugha mbili?

A Wahidiya B Thaniya
C Mahuluti D Rubaia

B

(x) Maelezo yapi yanafafanua kwa usahihi dhana ya mofimu?

A Kipashio kinachojitosheleza kileksika au kisarufi.
B Kipashio kinachojitosheleza kimuundo au kileksika.
C Kipashio kinachojitosheleza kimuundo au kisarufi.
D Kipashio kinachounda msamiati au maneno.

A

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 1.

Katika Kielelezo Na.1.1, mwanafunzi aliweza kuchagua herufi za majibu sahihi kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa mada zilizopimwa katika swali hili. Uchambuzi zaidi wa namna wanafunzi walivyojibu vipengele mbalimbali vya swali hili umefafanuliwa kama ifuatavyo:

(i) Ni methali ipi inayofanana na methali inayosema, "Mtaka cha uvunguni sharti ainame"?

A Ujanja mwingi mbele giza.
B Mjumbe hauawi.
C Akili nyingi huondoa maarifa.
D Atangae sana na jua hujua.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Tanzu za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima kukumbuka vipera vya tanzu za fasihi simulizi. Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi *D Atangae sana na jua hujua,* ambayo ni methali inayofanana na methali inayosema, "Mtaka cha

uvunguni sharti ainame". Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa kipera cha methali.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi katika kipengele hiki walishindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuchagua vipotoshi *A Ujanja mwingi mbele giza; B Mjumbe hauawi;* na *C Akili nyingi huondoa maarifa.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana anuai za methali husika hivyo kushindwa kubaini methali inayofanana na methali isemayo "Mtaka cha uvunguni sharti ainame" yenye maana ya *atakaye kitu kilicho mvunguni mwa kitanda lazima ainame ili kukichukua*. Uchaguzi wa vipotoshi *Ujanja mwingi mbele giza*; *Mjumbe hauawi*; na *Akili nyingi huondoa maarifa* ulitokana na wanafunzi hao kutojua maana za msingi za methali hizo ambazo ni *ujanja au werevu mwingi hufuatiwa na giza*, *apelekaye ujumbe fulani mahali hauawi* na *werevu mwingi huweza kuondoa busara na kuishia kuharibu* mtawalia. Hivyo, methali zilizopo katika vipotoshi A, B, na C hazifanani na methali waliyopewa.

(ii) Bainisha ubora wa kuhifadhi kazi za fasihi kwa kutumia njia ya picha na vinasa sauti.

A Fanani na hadhira huonana ana kwa ana.
B Wasanii huonekana dhahiri.
C Huwa na gharama ya kumiliki.
D Huweza kupotea na kutopatikana tena.

Swali lilitoka katika mada ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutathmini ubora wa njia za uhifadhi wa kazi za fasihi hususani kwa kutumia picha na vinasa-sauti. Wanafunzi waliokuwa na umahiri wa njia mbalimbali za kuhifadhi kazi za fasihi walichagua herufi ya jibu sahihi B *Wasanii huonekana dhahiri*. Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ubora wa picha na vinasa-sauti kama njia mojawapo ya kuhifadhi kazi za fasihi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walichagua vipotoshi A *Fanani na hadhira huonana ana kwa ana; C Huwa na gharama ya kumiliki*; na *D Huweza kupotea na kutopatikana tena*. Uchaguzi wa vipotoshi *Fanani na hadhira huonana ana kwa ana* na *Huwa na gharama ya kumiliki* ulitokana na wanafunzi hao

kutoelewa kuwa hizo ni sifa anuai za fasihi simulizi hazihusiki na ubora wa njia za kuhifadhi kazi za fasihi hususani picha na vinasa sauti. Aidha, uteuzi wa kipotoshi *Huweza kupotea na kutopatikana tena* ulitokana na kutojua kuwa hii ni hasara ya uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi kwa njia ya kichwa. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unatokana na wanafunzi hao kukosa uelewa wa njia mbalimbali za uhifadhi wa kazi za fasihi kwa ujumla.

(iii) Mwalimu aliwaagiza wanafunzi wawili wajibizane kishairi mbele ya wenzao darasani. Ni kipera kipi kinawakilisha walichofanya wanafunzi hao?

A Ngonjera
B Majigambo
C Kichekesho
D Igizo

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kukumbuka vipera vya fasihi simulizi vinavyotumia lugha ya kishairi katika utunzi na uwasilishaji wake. Baadhi ya wanafunzi walifanya vizuri swali hili kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi A *Ngonjera* kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa vipera vya tanzu za fasihi simulizi.

Hata hivyo, baadhi yao walichagua vipotoshi *B Majigambo*, *C Kichekesho*, na *D Igizo*. Uteuzi wa vipera hivyo ulitokana na wanafunzi kukosa uelewa wa vipera vya utanzu wa sanaa za maonesho ambavyo kiuhalisia huweza kutumia majibizano yasiyotumia lugha ya kishairi.

(iv) Sentensi ipi kati ya zifuatazo imeundwa na kitenzi kishirikishi?

A Tanzania ilikuwa inapendeza toka zamani.
B Watoto wanalima shamba dogo sana.
C Watu wa mjini si wengi kama wa vijijini.
D Mto mdogo umejaa majani mengi.

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na mada ndogo ya *Ubainishaji wa Aina za Maneno*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua sentensi iliyoundwa na kitenzi kishirikishi kati ya sentensi alizopewa. Baadhi ya wanafunzi waliokuwa na umahiri kuhusu dhana ya vitenzi na aina zake walichagua herufi ya jibu sahihi *C Watu wa mjini si wengi kama wa vijijini* kuwa ndiyo sentensi iliyoundwa na kitenzi kishirikishi (*si*).

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walishindwa kujibu swali hili kwa kuchagua vipotoshi *A Tanzania ilikuwa inapendeza toka* zamani, *B Watoto wanalima shamba dogo sana;* na *D Mto mdogo umajaa majani mengi*. Wanafunzi hao walionesha kutokuwa na uelewa wa kutosha wa vitenzi vishirikishi. Uchaguzi wa kipotoshi A ulitokana na wanafunzi hao kushindwa kutofautisha kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu kwani sentensi hiyo iliundwa na kitenzi kisaidizi (Ts) *ilikuwa* na kitenzi kikuu (T) *inapendeza*. Vilevile, uchaguzi wa vipotoshi B na D ulitokana na wanafunzi kushindwa kutambua kuwa sentensi hizo ziliundwa na vitenzi vikuu *wanalima* na *umejaa* badala ya vitenzi vishirikishi kama swali lilivyotaka.

(v) Sauti ya lugha inayotamkwa bila kuwapo na kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa huitwaje?

A Silabu
B Irabu
C Konsonanti
D Mkazo

Swali lilitoka katika mada ya *Mawasiliano* hususani mada ndogo ya *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili.* Swali lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu sauti za lugha. Miongoni mwa wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi B *Irabu* kutokana na kuwa na uelewa wa ala za matamshi. Umahiri huo uliwawezesha wanafunzi hao kubaini kwa usahihi sauti ya lugha inayotamkwa bila kuwepo kwa kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa ambayo ni *irabu*.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walijibu vibaya swali hili kwa kuchagua vipotoshi *A Silabu*, *C Konsonanti*, na *D Mkazo* kutokana na kukosa umahiri kuhusu sauti za lugha. Uchaguzi wa kipotoshi

*Silabu* ulitokana na wanafunzi hao kuchanganya neno hilo na *Silabi*, ambayo ni sehemu ya neno inayoundwa kwa irabu au konsonanti na irabu na hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Uchaguzi wa kipotoshi *Konsonanti* ulitokana na wanafunzi hao kushindwa kubaini sauti hiyo inayotamkwa kwa kubana au kuzuia mkondo wa hewa. Vivyo hivyo uchaguzi wa kipotoshi *Mkazo* ulitokana na kushindwa kutambua kuwa mkazo ni kiwango cha nguvu inayotumika katika utamkaji wa silabi na si sauti. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo kwa ujumla unatokana na wanafunzi hao kukosa uelewa wa sauti mbalimbali na jinsi zinavotumika katika lugha.

(vi) Mojawapo ya alama za uandishi ni nukta. Kazi ya alama hiyo ni ipi katika sentensi?

A Kukariri au kurudia maneno yaliyosemwa.
B Kuonesha sentensi imefikia mwisho na imekamilika.
C Kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume.
D Kuashiria maneno yaliyo kwenye orodha.

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi* hususani mada ndogo ya *Uandishi wa Insha* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutambua alama za uandishi na matumizi yake katika sentensi. Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *B Kuonesha sentensi imefika mwisho na imekamilika*. Uchaguzi huu unaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kutosha wa matumizi ya alama mbalimbali za uandishi hususani nukta ambayo kazi yake ni kukamilisha sentensi.

Hata hivyo, wanafunzi wengine walichagua vipotoshi *A Kukariri au kurudia maneno yaliyosemwa*; *C Kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume;* na *D Kuashiria maneno yaliyo kwenye orodha*. Uteuzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi hao kukosa uelewa wa alama za uandishi na matumizi yake katika sentensi. Kipotoshi *Kukariri au kurudia maneno yaliyosemwa* ni nukuu na si alama ya uandishi. Uchaguzi wa kipotoshi *Kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume* ulitokana na kutoelewa kuwa dhana hii huhusu visawe na si nukta. Vilevile, uchaguzi wa kipotoshi *Kuashiria maneno yaliyo kwenye orodha* ulitokana na wanafunzi hao kuchanganya matumizi ya nukta (**.**) na nuktapacha (**:**), ambayo huashiria maneno yaliyo kwenye orodha katika sentensi.

(vii) Mwalimu aliwataka wanafunzi kuchambua neno "**anacheza**" na kuonesha viambishi vyake. Uchambuzi upi unaonesha mpangilio sahihi wa viambishi?

A Kiambishi awali ni **a-**, **-na-** na kiambishi tamati ni **-a**.
B Kiambishi awali ni –a na kiambishi tamati ni -na.
C Kiambishi awali ni –na- na tamati ni -a.
D Kiambishi awali ni **–na-** na –**chez**- na tamati nia **a-**.

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* hususani mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji.* Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika uundaji wa maneno kwa kutumia uambishaji. Wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *A Kiambishi awali ni* ***a-, -na-*** *na kiambishi tamati ni* ***-a*** ambao ni mpangilio sahihi wa viambishi katika neno **"anacheza**." Wanafunzi hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uambishaji katika mzizi wa neno.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi wengine walichagua vipotoshi *B Kiambishi awali ni* ***–a*** *na kiambishi tamati ni* **–na-**, ambapo ***–na-*** ni kiambishi awali cha njeo na si kiambishi tamati. Kipotoshi *C Kiambishi awali ni* ***-na-*** *na tamati ni* ***a-***, ambapo viambishi awali katika neno "**anacheza**" ni **a-** na **–na-** na si **–na-** peke yake. Vilevile, kipotoshi *D Kiambishi awali ni* ***–na-*** *na* ***–chez-*** *na tamati ni* ***a-***, ambapo kiambishi awali ni **a-** na -**na**- lakini -**chez**- ni mzizi wa neno na si kiambishi awali cha neno **anacheza**.

Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa wanafunzi hao walikosa umahiri wa kutumia viambishi awali na tamati katika neno **'anacheza**' hivyo kushindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.

(viii) Kisawe cha neno "jokofu" ni kipi kati ya hivi?

A Jiko
B Tanuru
C Friji
D Stovu

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* na mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi.* Swali lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi wa kutambua visawe vya maneno mbalimbali, hivyo

kuchagua herufi ya jibu sahihi C *Friji* ambacho ni kisawe cha neno "jokofu" lenye maana ya chombo kinachotumika kupoza vitu vilivyohifadhiwa ndani yake.

Wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili walichagua vipotoshi A *Jiko*; B *Tanuru;* na D *Stovu.* Wanafunzi waliochagua kipotoshi *Jiko* walishindwa kujua kuwa hiki ni kifaa au mahali panapotumika kupikia au kuandaa chakula. Uteuzi wa kipotoshi *Tanuru* ulitokana na kutojua kuwa ni aina ya jiko linalotumika kuokea mikate au kuchomea mkaa au matofali. Adha, uchaguzi wa kipotoshi *Stovu* ulitokana na kutokuelewa kuwa ni jiko linalotumia mafuta ya taa. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi hao kukosa uelewa wa maneno yenye maana sawa au visawe hivyo kushindwa kubaini kisawe cha neno jokofu kuwa ni *friji*.

(ix) Aina ipi ya kamusi hutumia lugha mbili?
A Wahidiya
B Thaniya
C Mahuluti
D Rubaia

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* hususani mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi* na lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu aina ya kamusi inayotumia lugha mbili. Wanafunzi waliojibu vizuri swali hili walichagua jibu sahihi *B Thaniya* ambayo ni aina ya kamusi inayotumia lugha mbili. Wanafunzi hawa walikuwa na maarifa ya kutosha ya kutambua aina mbalimbali za kamusi.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi walichagua vipotoshi *A Wahidiya*, *C Mahuluti*, na *D Rubaia* kutokana na kukosa umahiri wa kutumia kamusi. Uchaguzi wa kipotoshi *Wahidiya* ulitokana na kutotambua kuwa hii ni aina ya kamusi inayotumia lugha moja. Waliochagua kipotoshi *Mahuluti* walishindwa kutambua kuwa hii ni aina ya kamusi inayotumia lugha tatu. Vilevile, waliochagua kipotoshi *Rubaia* walishindwa kutambua kuwa hakuna kamusi ya aina hiyo katika lugha ya Kiswahili.

(x) Maelezo yapi yanafafanua kwa usahihi dhana ya mofimu?
   A Kipashio kinachojitosheleza kileksika au kisarufi.
   B Kipashio kinachojitosheleza kimuundo au kileksika.
   C Kipashio kinachojitosheleza kimuundo na kisarufi.
   D Kipashio kinachounda msamiati au maneno.

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* hususani mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji* na lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu maumbo mbalimbali ya maneno katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wanafunzi walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mofimu kwani walichagua herufi ya jibu sahihi A *Kipashio kinachojitosheleza kileksika au kisarufi*.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi walichagua vipotoshi *B Kipashio kinachojitosheleza kimuundo au kileksika*; *C Kipashio kinachojitosheleza kimuundo au kisarufi;* na *D Kipashio kinachounda msamiati au maneno*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na wanafunzi hao kukosa umahiri kuhusu dhana ya mofimu kwa ujumla. Vipotoshi *B, C,* na *D* havifafanui kwa usahihi dhana ya mofimu kwani katika vipotoshi B na C dhana ya kisarufi au kileksika imechanganywa na utoshelevu wa kimuundo ambao kiuhalisia ni kipengele kimojawapo kinachopatikana ndani ya sarufi. M*ofimu* ni kipengele chenye utoshelevu wa kisarufi kinachohusisha matamshi, maana, maumbo na mpangilio wa maneno wenye kuleta maana (kileksika). Uchaguzi wa kipotoshi *D* si ufafanuzi sahihi wa mofimu kwani *msamiati* ni seti ya maneno yote katika lugha. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyechagua herufi za majibu yasiyo sahihi katika vipengele 9 na kupata alama za chini.

**SEHEMU A (Alama 15)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika vipengele (i) hadi (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Ni methali ipi inayofanana na methali inayosema, "Mtaka cha uvunguni sharti ainame"?

A Ujanja mwingi mbele giza.
B Mjumbe hauawi.
C Akili nyingi huondoa maarifa.
D Atangae sana na jua hujua.

[B]

(ii) Bainisha ubora wa kuhifadhi kazi za fasihi kwa kutumia njia ya picha na vinasa sauti.

A Fanani na hadhira huonana ana kwa ana.
B Wasanii huonekana dhahiri.
C Huwa na gharama ya kumiliki.
D Huweza kupotea na kutopatikana tena.

[D]

(iii) Mwalimu aliwaagiza wanafunzi wawili wajibizane kishairi mbele ya wenzao darasani. Ni kipera kipi kinawakilisha walichofanya wanafunzi hao?

A Ngonjera B Majigambo
C Kichekesho D Igizo

[B]

(iv) Sentensi ipi kati ya zifuatazo imeundwa kwa kitenzi kishirikishi?

A Tanzania ilikuwa inapendeza toka zamani.
B Watoto wanalima shamba dogo sana.
C Watu wa mjini si wengi kama wa vijijini.
D Mto mdogo umejaa majani mengi.

[B]

(v) Sauti ya lugha inayotamkwa bila kuwapo na kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa huitwaje?

A Silabu B Irabu
C Konsonanti D Mkazo

[A]

(vi) Mojawapo ya alama za uandishi ni nukta. Kazi ya alama hiyo ni ipi katika sentensi?

A Kukariri au kurudia maneno yaliyosemwa.
B Kuonesha sentensi imefikia mwisho na imekamilika.
C Kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume.
D Kuashiria maneno yaliyo kwenye orodha.

[B]

(vii) Mwalimu aliwataka wanafunzi kuchambua neno "**anacheza**" na kuonesha viambishi vyake. Uchambuzi upi unaonesha mpangalio sahihi wa viambishi?

A Kiambishi awali ni ***a***-, -***na***- na kiambishi tamati ni –***a***
B Kiambishi awali ni –**a** na kiambishi tamati ni –**na**-
C Kiambishi awali ni –**na**- na tamati ni **a-**
D Kiambishi awali ni –***na***- na – ***chez*** – na tamati ni ***a***-

[B]

(viii) Kisawe cha neno "jokofu" ni kipi kati ya hivi?

A Jiko B Tanuru
C Friji D Stovu

[B]

(ix) Aina ipi ya kamusi hutumia lugha mbili?

A Wahidiya B Thaniya
C Mahuluti D Rubaia

[C]

(x) Maelezo yapi yanafafanua kwa usahihi dhana ya mofimu?

A Kipashio kinachojitosheleza kileksika au kisarufi.
B Kipashio kinachojitosheleza kimuundo au kileksika.
C Kipashio kinachojitosheleza kimuundo au kisarufi.
D Kipashio kinachounda msamiati au maneno.

[C]

Kielelezo Na. 1.2: *Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 1*

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele 9 na kupata alama 01 kati ya alama 10 za swali hili.

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha


Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uelewa wa wanafunzi wa kutambua maana za vipera vya tanzu za fasihi simulizi. Swali liliuliza:

> *Oanisha maana za tanzu za fasihi simulizi zilizopo katika* ***Orodha*** **A** *na tanzu husika kutoka* ***Orodha*** **B**, *kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.*

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (i) Tungo yenye mpangilio mzuri wa silabu na lugha ya mkato.<br>(ii) Tungo zenye muundo wa mashairi ya kimapokeo.<br>(iii) Maigizo yanayohusu mambo mbalimbali ya kishujaa.<br>(iv) Tungo zenye mpangilio wa silabi zinazolingana kwa kila mstari.<br>(v) Mpangilio wa maneno unaombatana na utendaji wa wahusika. | A Majigambo<br>B Ngonjera<br>C Tenzi<br>D Ushairi<br>E Nyimbo<br>F Maigizo<br>G Utani |

Swali lilikuwa na vipengele vitano, ambapo mwanafunzi alitakiwa kuoanisha maana za tanzu za fasihi simulizi zilizopo katika Orodha A na tanzu husika kutoka Orodha B.

Wanafunzi 695,261 sawa na asilimia 99.99 waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa wanafunzi katika swali hili unaonesha kuwa ulikuwa wa wastani ambapo asilimia 62.67 walifaulu kwa viwango vya wastani na kizuri. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 104,144 (14.98%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 4 hadi 5, wanafunzi 331,599 (47.69%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 2 hadi 3 na wanafunzi 259,518 (37.33%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 1.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 331,599 sawa na asilimia 47.69 walikuwa na ufaulu wa wastani kutokana na kumudu kutoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipera vya tanzu za fasihi simulizi na kushindwa katika vipera vingine. Wanafunzi hao walioanisha kwa usahihi vipengele 2 hadi 3 vya swali na kushindwa katika vipengele vingine, hivyo kupata alama kati ya 2 na 3. Wanafunzi hao walionesha kuwa na maarifa yasiyojitosheleza kuhusu maana anuai za tanzu za fasihi simulizi kwani baadhi yao walichanganya maana za tanzu hizo hususani nyimbo na ushairi hatimaye kuoanisha kimakosa.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 104,144 sawa na asilimia 14.98 walikuwa na ufaulu mzuri kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa tanzu za fasihi simulizi. Wanafunzi hao waliweza kuoanisha kwa usahihi maana za tanzu za fasihi simulizi zilizopo katika Orodha A na tanzu husika kutoka Orodha B na kupata alama za juu kati ya 4 na 5. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa ya swali.

2. Oanisha maana za tanzu za fasihi simulizi zilizopo katika **Orodha A** na tanzu husika kutoka **Orodha B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Tungo yenye mpangilio mzuri wa silabi na lugha ya mkato. | A Majigambo |
| (ii) Tungo zenye muundo wa mashairi ya kimapokeo. | B Ngonjera |
| (iii) Maigizo yanayohusu mambo mbalimbali ya kishujaa. | C Tenzi |
| (iv) Tungo zenye mpangilio wa silabi zinazolingana kwa kila mstari. | D Ushairi |
| (v) Mpangilio wa maneno unaoambatana na utendaji wa wahusika. | E Nyimbo |
| | F Maigizo |
| | G Utani |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | D | B | A | C | F |

Kielelezo Na. 2.1: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2*

Katika Kielelezo Na. 2.1, mwanafunzi alioanisha kwa usahihi maana za tanzu za fasihi simulizi zilizopo katika Orodha A na tanzu husika kutoka Orodha B.

Hata hivyo, wanafunzi 259,518 sawa na asilimia 37.33 waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kati ya 0 na 1. Hii ni kutokana na kukosa uelewa wa kutosha wa tanzu za fasihi simulizi, hivyo kushindwa kuoanisha kwa usahihi maana ya tanzu za fasihi simulizi zilizopo katika Orodha A na tanzu husika kutoka Orodha B. Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi hao walishindwa kutambua maana za tanzu za fasihi simulizi hususani *ushairi* ambayo ni tungo yenye mpangilio mzuri wa silabi na lugha ya mkato; *ngonjera* ni tungo zenye mpangilio wa kimapokeo; *majigambo* ni maigizo yanayohusu mambo mbalimbali ya kishujaa; *tenzi* ni tungo zenye mpangilio wa silabi zinazolingana kwa kila mstari; na *maigizo* ni mpangilio wa maneno unaoambatana na utendaji wa wahusika. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vibaya swali hili na kupata 0.

2. Oanisha maana za tanzu za fasihi simulizi zilizopo katika **Orodha A** na tanzu husika kutoka **Orodha B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Tungo yenye mpangilio mzuri wa silabi na lugha ya mkato. | A Majigambo |
| | B Ngonjera |
| (ii) Tungo zenye muundo wa mashairi ya kimapokeo. | C Tenzi |
| (iii) Maigizo yanayohusu mambo mbalimbali ya kishujaa. | D Ushairi |
| | E Nyimbo |
| (iv) Tungo zenye mpangilio wa silabi zinazolingana kwa kila mstari. | F Maigizo |
| | G Utani |
| (v) Mpangilio wa maneno unaoambatana na utendaji wa wahusika. | |

**Majibu**

| **Orodha A** | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Orodha B** | C | E | F | D | A |

Kielelezo Na. 2.2: *Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 2*

Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeoanisha kwa makosa maana zote za tanzu za fasihi simulizi katika Orodha A na tanzu husika kutoka Orodha B na kupata 0.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba (7) ya majibu mafupi. Kila swali lilikuwa na alama kumi (10) na kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama 70. Maswali yaliyopimwa katika sehemu hii yalihusu mada za *Ufahamu, Aina za Maneno, Mawasiliano, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali,* na *Fasihi kwa Ujumla*.

### 2.2.1 Swali la 3: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* hususani mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma Kimya* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukumbuka mawazo ya mwandishi katika kifungu cha habari. Swali lilimtaka mwanafunzi kusoma kifungu cha habari alichopewa kisha kujibu maswali yanayofuata. Kifuatacho ni kifungu cha habari alichopewa.

*Ulimwengu ni sawa na kitabu kikubwa ambacho juu ya ukubwa wote kurasa zake ni mbili, nazo ni furaha na huzuni. Mwanadamu katika safari yake ya maisha hapa duniani,* ***hana budi*** *kusoma kurasa zote mbili. Kwa mujibu wa maumbile, kila mwanadamu angependelea sana kudumu na ukurasa wa furaha, lakini matarajio haya hayapati kuwatokea waombaji. Badala yake huletewa kurasa hizo mbili kwa zamu. Ni dhahiri kwamba sisi sote tunajua kwamba kurasa hizi hazikwepeki na hatuna budi tuzisome.*


*Kama tulivyokuwa na majaliwa ya namna mbalimbali,* ***imedhihirika*** *kwamba kuna wengine wamejaliwa kusoma ukurasa wa furaha kwa muda mrefu kuliko kusoma wa huzuni. Pia, kuna wale ambao kujaliwa kwao kumewafungulia ukurasa ule wa pili wa kusoma kwa muda mrefu zaidi kuliko wa kwanza. Tena, hapana shaka kwamba wapo waliojaliwa kupata huku na huku, sawasawa. Hivyo kila mmoja hana budi kuonja kurasa zote mbili.*

*Endapo kungetokea nafasi ya kuchagua ukurasa uupendao kusoma, bila shaka kila mmoja wetu angechagua ukurasa wa furaha. Lakini uchaguzi huu usingekuwa na tija kwa sababu watu wa kundi hili wangejua kwamba duniani kuna furaha tu na hakuna ambaye angeweza* ***kuwarudi*** *wanapofanya kufuru. Aidha, wasingewafikiria wenzao wenye huzuni na kuwafariji. Vilevile kama mmojawapo angekosea akachagua huzuni tu, pia angejihisi kuwa ni mnyonge sana katika jamii kwa sababu yeye angeishi maisha* ***yaliyogubikwa*** *na huzuni tu, wala furaha isingepata nafasi katika maisha yake.*

*Hali kama hii ingeleta watu kubaguana na kutosaidiana* ***asilani,*** *kusingekuwa na watu* ***rahimu.*** *Kwani, mwenye furaha angehisi nini mpaka amsaidie mwenye huzuni? Furaha na huzuni vinashabihiana katika maisha ya binadamu, utajiona una huzuni kwa sababu huna furaha, hivyo hivyo kwa mwenye furaha. Kauli mbiu ni kwamba "furaha na huzuni ni sehemu ya maisha" kubali matokeo ya hali ya maisha inayojitokeza.*

Kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi kuandika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari aliyosoma kisichozidi maneno matano. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kueleza sababu za mwandishi kusisitiza umuhimu wa kila mmoja kusoma kurasa zote mbili za kitabu. Kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kueleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari aliyosoma *(i) Hana budi, (ii) Imedhihirika, (iii) Yaliyoghubikwa, (iv) Asilani* na *(v) Kuwarudi.* Kipengele (d) kilimtaka mwanafunzi kuandika funzo alilolipata katika habari aliyosoma.

Wanafunzi 695,268 sawa na asilimia 100 ya waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo asilimia 70.52 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 3:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 119,434 (17.18%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 370,841 (53.34%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wanafunzi 204,993 (29.48%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Uchambuzi wa ufaulu unaonesha kuwa, idadi kubwa ya wanafunzi sawa na 53.34 walikuwa na ufaulu wa wastani kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele

vingine. Wanafunzi hao walijibu kwa usahihi vipengele 3 hadi 6. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika kwa usahihi kichwa cha habari kinachoendana na habari aliyosoma kwa maneno yasiyozidi matano kama vile (a) FURAHA NA HUZUNI KATIKA MAISHA; kipengele (c) alieleza kwa usahihi maana ya maneno aliyopewa kama vile (i) *Hana hiari,* (iii) *tawaliwa*, na (v) *kuwaonya*; lakini alishindwa kujibu kwa usahihi kipengele (b) na (d) hivyo kuwa na ufaulu wa wastani.

Aidha, wanafunzi 119,434 sawa na asilimia 17.18 walijibu vizuri swali hili kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vingi na kupata alama za juu kati ya 6.5 na 10. Uchambuzi wa majibu yao unaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kutosha wa mada ya *Ufahamu*. Asilimia 0.6 walijibu kwa usahihi vipengele vyote vinne (a) hadi (d) na kupata alama zote 10. Katika kipengele (a) waliandika kichwa cha habari sahihi kulingana na habari waliyosoma kama vile ULIMWENGU WA FURAHA NA HUZUNI, MAISHA YA MWANADAMU HAPA DUNIANI, KURASA ZA KITABU CHA MAISHA, NYAKATI KUU MBILI KATIKA MAISHA, KURASA MBILI ZA MAISHA na FURAHA NA HUZUNI KATIKA MAISHA. Katika kipengele (b) waliandika majibu sahihi kama vile : *Kila mmoja lazima aonje furaha na huzuni/furaha na huzuni ni sehemu ya maisha ya mwanadamu*. Katika kipengele (c) walieleza kwa usahihi maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari kama vile: (i) Hana budi (*hana hiari au ni lazima*), (ii) Imedhihirika (*imefahamika, imeonekana au imebainika*), (iii) Yaliyoghubikwa (*zongwa au tawaliwa*), (iv) Asilani (*kabisa, kamwe, hata kidogo au katu*, na (v) Kuwarudi (*kuwaonya au kuwaadhibu*). Katika kipengele (d) waliandika funzo sahihi linalopatikana katika kifungu cha habari hii kuwa, *maisha ya binadamu katika ulimwengu yana sehemu mbili, yaani tabu na raha.* Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote 10.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano....FURAHA NA HUZUNI NI MAISHA....

............

(b) Kwa nini mwandishi anasisitiza umuhimu wa kila mmoja kusoma kurasa zote mbili za kitabu?...Ni muhimu kusoma kurasa mbili za kitabu kwani furaha na huzuni zote ni sehemu za maisha ya mwanadamu katika safari yake ya maisha hapa duniani

(c) Eleza maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Hana budi.........
Ni lazima na muhimu mtu kutekeleza jambo fulani
............

(ii) Imedhihirika.........
Ni kuonekana na kugundulika kwa kitu fulani.
............

(iii) Yaliyogubikwa.........
Ni hali ya kutawaliwa na kitu fulani
............

(iv) Asilani.........
Ni hali au kitendo cha kutofanya kitu kabisa na kamwe

(v) Kuwarudi.........
Ni hali ya mtu kuonywa, kuaswa ~~na kushauriwa~~ baada ya kufanya jambo fulani.

(d) Andika funzo unalopata katika habari hii.
Nimepata funzo kuwa ni vizuri binadamu kupitia nyakati za furaha na huzuni katika maisha ili aweze kujenga hali ya kuwasaidia wengine wakiwa katika huzuni na kuwafariji na kujenga hali ya kutobaguana.

Kielelezo Na. 3.1: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 3*

Katika Kielelezo Na. 3.1, mwanafunzi alijibu vizuri vipengele vyote vinne kwa kuandika katika (a) kichwa cha habari kwa herufi kubwa na kisichozidi maneno matano, (b) umuhimu wa kila binadamu

kusoma kurasa zote za kitabu yaani kuyakubali maisha nyakati za furaha na huzuni, (c) maana sahihi za maneno aliyopewa kama yalivyotumika katika habari, na (d) funzo linalopatikana katika habari aliyosoma.

Hata hivyo, asilimia 29.48 ya wanafunzi walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 2.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya mada ya *Ufahamu*. Wanafunzi hao walishindwa kujibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali hili na kujibu kwa usahihi kipengele kimoja au viwili na wengine kushindwa kabisa kujibu vipengele vyote vinne (a) hadi (d). Kutokana na kukosa uelewa wa kifungu cha habari, baadhi ya wanafunzi hao walitoa majibu yasiyo sahihi hususani kutumia baadhi ya maneno katika habari na kuyafanya kichwa cha habari, kwa mfano mwanafunzi mmoja aliandika *KUBAGUANA*. Katika kipengele (b) walitoa sababu zisizo sahihi kuhusu umuhimu wa kila mmoja kusoma kurasa zote mbili za kitabu ambapo mwanafunzi mwingine aliandika sababu mojawapo ni *kufurahia maisha*. Katika kipengele (c), wanafunzi walishindwa kuandika kwa usahihi maana za maneno waliyopewa kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Baadhi walinukuu maneno hayo, na wengine walitunga sentensi kwa kutumia maneno hayo. Katika kipengele (d), wanafunzi walishindwa kuandika funzo linalopatikana katika habari waliyosoma. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alikanusha kuwa hakuna funzo lolote katika habari hii kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu vipengele vyote vya swali hili.

**Maswali**

(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyosoma kisichozidi maneno matano. MAISHA YA MWANADAMU.

(b) Kwa nini mwandishi anasisitiza umuhimu wa kila mmoja kusoma kurasa zote mbili za kitabu? Ili kuweza kutambua dhiki na faraja katika maisha ya mwanadamu

(c) Eleza maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Hana budi ni neno linalo simama badala ya neno yampasa mtu kufanya kitu katika jambo fulani

(ii) Imedhihirika ni neno Linalo simama badala ya neno imetambulika

(iii) Yaliyogubikwa ni neno linalosimama badala ya neno kujawa. Mfano wa katika habari ni kujawa na huzuni

(iv) Asilani ni neno linaloweza kusimama badala ya neno shida. Mfano wa katika habari ni watu kuba guana na kutosaidiana kwenye shida.

(v) Kuwarudi ni neno linalosimama badala ya neno kurudi kwa ajili ya watu fulani.

(d) Andika funzo unalopata katika habari hii.
Nimepata funzo ya kwamba maisha ya mwana damu ni yapande mbili kwasababu baada ya kuzaliwa pia kuna maisha baada ya kifo.


Kielelezo Na. 3.2: *Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 3*

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafuzni aliyeshindwa kujibu vipengele vyote vinne (a) – (d) vya swali hili kwa kutoa majibu yasiyolingana na matakwa ya swali na kupata 0.

### 2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* hususani mada ndogo ya *Matumizi ya Aina za Maneno katika Tungo.* Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi kuhusu matumizi sahihi ya aina za maneno katika tungo. Swali lilimtaka mwanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa ili kuwakilisha aina husika za maneno aliyopewa katika vipengele husika.

Wanafunzi 695,267 sawa na asilimia 99.99 ya waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo wanafunzi 672,159 sawa na asilimia 96.67 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kiasilimia.





**Chati Na. 4***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 559,782 (80.51%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 112,377 (16.16%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wanafunzi 23,108 (3.32%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama kati ya 0 hadi 2.5.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri, ambapo wanafunzi 559,782 sawa na asilimia 80.51 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10. Aidha, wanafunzi 355,148 sawa na asilimia 51.1 walipata alama zote 10 kutokana na kuwa na

uelewa wa kutosha kuhusu matumizi sahihi ya aina za maneno katika tungo. Wanafunzi hao waliweza kutunga kwa usahihi sentensi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa ili kuwakilisha aina husika za maneno katika vipengele (a) hadi (e). Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitunga sentensi zifuatazo: ***Mimi** ni mwanafunzi mstaarabu sana*; (b) *Shamba **letu** ni kubwa sana*; (c) *Sisi **tutaendelea** kusoma kwa bidii;* (d) *Baba **na** mama wanakula*; na (e) *Asha ana **upendo** kwa wazazi wake.* Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama zote 10.



4. Tunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa ili kuwakilisha aina husika za maneno:
Mfano: **Jana usiku** litumike kama kielezi.
Sentensi: Wote wawili waliondoka **jana usiku**.

(a) **Mimi** litumike kama kiwakilishi.
Mimi ni mwanafunzi wa kidato cha pili.

(b) **Letu** litumike kama kivumishi.
Gari letu limeharibika.

(c) **Tutaendelea** litumike kama kitenzi kisaidizi.
Sisi tutaendelea kusoma kwa bidii.

(d) **Na** litumike kama kiunganishi.
Baba na mama wanalima shambani.

(e) **Upendo** litumike kama nomino dhahania.
Upendo baina ya wanafamilia ni muhimu.

Kielelezo Na. 4.1: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4*

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyetunga kwa usahihi sentensi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa (*mimi, letu, tutaendelea, na* na *upendo*) ili kuwakilisha aina husika za maneno katika vipengele (a) hadi (e).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi wengine 112,377 sawa na asilimia 16.16 walikuwa na ufaulu wa wastani kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele husika. Wanafunzi hao walitunga sentensi kwa usahihi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa ili kuwakilisha aina husika za maneno katika vipengele 2 hadi 3 na kushindwa kutunga sentensi zingine, hivyo kupata alama za wastani kati ya 3 hadi 6.

Licha ya swali hili kuwa na ufaulu mzuri, wanafunzi 23,108 sawa na asilimia 3.32 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata kati ya alama 0 na 2.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Matumizi ya Aina za Maneno katika Tungo*. Ufaulu hafifu ni ishara kuwa wanafunzi hao walikosa uelewa wa aina za maneno, hivyo kushindwa kutambua aina sahihi za maneno husika. Wanafunzi wengi katika kundi hili waliweza kutunga sentensi moja na wengine walishindwa kutunga sentensi hata moja kutokana na kukosa umahiri wa kuunda sentensi za Kiswahili, hivyo kupata alama hafifu. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitunga sentensi zisizozingatia sintaksia ya Kiswahili kama vile: (a) *Jana nilikula chakula mimi*. Sentensi hii ilikiuka sintaksia ya Kiswahili ambapo muundo sahihi ulipaswa kuwa **Mimi nilikula chakula jana**. Mwanafunzi mwingine katika kipengele (b) aliandika *Gari limeua watu letu* badala ya **Gari letu limeua watu**. Katika (c) aliandika *Shamba kulima kesho tutaendelea*; ambapo alishindwa kubaini kuwa kitenzi kisaidizi hakiwezi kuwa mwishoni mwa sentensi au kutanguliwa na kitenzi kikuu. Sentensi ilitakiwa kuandikwa **Tutaendelea kulima shamba kesho**. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kutunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa katika vipengele vyote yaani (a) hadi (e) na kupata 0.

4. Tunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa ili kuwakilisha aina husika za maneno:
Mfano: **Jana usiku** litumike kama kielezi.
Sentensi: Wote wawili waliondoka **jana usiku**.

(a) **Mimi** litumike kama kiwakilishi.
Utumike kama kiwakilishi mimi

(b) **Letu** litumike kama kivumishi.
Utumike kama kiwakilishi letu

(c) **Tutaendelea** litumike kama kitenzi kisaidizi.
Tutaendelea kama kitenzi kisaidizi
kitumike

(d) **Na** litumike kama kiunganishi.
Utumike kama kiunganishi na

(e) **Upendo** litumike kama nomino dhahania.
Utumike kama nomino dhahania upendo


Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi ya Swali la 4

Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kutunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyokolezwa badala yake, alinakili maelekezo ya swali kwa kila kipengele na kupata 0.

### 2.2.3 Swali la 5: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* hususani mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kutumia kamusi ambapo alitakiwa kufafanua hatua tano za kuzingatia ili kupata maana ya maneno katika kamusi.


Wanafunzi 695,257 sawa na asilimia 99.99 ya waliofanya upimaji walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo wanafunzi 189,073 sawa na asilimia 27.19 pekee ndio waliofaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 5***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 16,516 (2.38%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 172,557 (24.82%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wanafunzi 506,184 (72.81%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata 0 hadi alama 2.5.

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili unaonesha kuwa wa chini ambapo zaidi ya asilimia 72.81 ya wanafunzi walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata kati ya alama 0 na 2.5. Ufaulu hafifu ulitokana na wanafunzi hao kukosa umahiri katika mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi*, hivyo kushindwa kufafanua hatua tano za kuzingatia ili kupata maana ya maneno katika kamusi. Takwimu za ufaulu zinaonesha kuwa, wanafunzi 221,916 sawa na asilimia 31.9 walishindwa kabisa kufafanua hatua hata moja hivyo kupata 0. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika umuhimu wa kamusi badala ya kufafanua hatua za kuzingatia ili kupata maana ya neno katika kamusi kwa kuandika katika kipengele (a) *Kuhifadhi misamiati ya lugha*, (b) *Kutoa fasili ya maneno mbalimbali*, (c) *Kutoa matamshi sahihi*, na (e) *Kutoa alama ya ufupisho*. Pia katika kipengele (d) aliandika *Kutoa maana asili ya neno* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali na kupata 0.



5. Fafanua hatua tano za kuzingatia ili kupata maana ya neno katika kamusi.

(a) Njia ya ukopaji
ni njia ya kuchukua au kuongeza neno ili iletee maana sahihi ya neno

(b) Uradidi / urudiaji
Ni ile hali ya kurudia rudia maneno mfano barabara.

(c) Njia ya usanifishaji
Njia hii hutumika katika kusanifisha maneno mapya kwenye kamusi

(d) Njia ya Uhohogji / kupunguza maneno
ni njia ambayo tuna punguza maneno ili iweze kuleta maana sahihi ya neno husika

(e) Njia ya unyambulishaji
Ni muhimu kwa sababu hutumika kunyambulish a maneno katika kamusi

Kielelezo Na. 5.1: *Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 172,557 sawa na asilimia 24.82 walikuwa na ufaulu wa wastani kutokana na kufafanua kwa usahihi baadhi ya hatua za kuzingatia ili kupata maana ya maneno katika kamusi na kushindwa kufafanua hatua zingine. Wanafunzi hao walionesha kuwa na umahiri usiojitosheleza kuhusu hatua za kufuata ili kupata maana katika kamusi, hivyo kumudu kufafanua hatua mbili hadi tatu na kupata alama 3 hadi 6.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 16,516 sawa na asilimia 2.38 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua za kuzingatia ili kupata maana ya maneno katika kamusi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alifafanua kwa usahihi hatua hizo kama vile: (a) *kutazama herufi ya mwanzoni katika kutafuta neno husika*; (b) *maneno yaliyo katika wingi kugeuza katika umoja*; (c) *kutafuta herufi za mwanzoni za neno kwa maneno yaliyoambatana*; (d) *Neno kutafuta mzizi katika neno lenye viambishi*; na (e) *kutafuta neno halisi kwa maneno yenye maana zaidi ya moja*. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa ya swali hivyo kupata alama za juu.

5. **Fafanua hatua tano za kuzingatia ili kupata maana ya neno katika kamusi.**

(a) Asili ya neno (Ethmology)
Kuwepo kwa asili ya neno ili kupata kujua neno lina asili ya wapi mfano : Shkamo – lina asili ya Uarabuni.

(b) Kuwepo kwa picha na Michoro.
Kuwepo kwa picha na Michoro, hukuza uelewa wa mtu katika neno fulani

(c) Kuwepo kwa visawe vya maneno.
Kuwepo kwa visawe na maneno hufanya watumiaji wa kamusi kujua neno linaloendana maana na jingine.

(d) Kuonesha utamkaji wa maneno.
ili kujua maana ya neno unatakiwa ujue jinsi linavyotamkwa. mfano mama - /mama/.

(e) Kuwepo kwa kitomeo na kidahizo.
Kuonesha neno alisia na maana ya neno hilo mfano ; Baba - mwanaume ambaye ana watoto kwenye familia.


Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyefafanua kwa usahihi hatua zote tano za kuzingatia ili kupata maana ya maneno katika kamusi na kupata alama zote 10.

### 2.2.4 Swali la 6: Mawasiliano

Swali lilitoka katika mada *ya Mawasiliano* hususani mada ndogo ya *Lugha kama Chombo cha Mawasiliano.* Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa kutumia lugha fasaha na lilimtaka kutoa hoja tano kuelezea umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii.

Wanafunzi 695,257 sawa na asilimia 99.99 ya waliofanya upimaji walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani, ambapo wanafunzi 243,394 sawa na asilimia 35.01 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.





**Chati Na. 6***: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 47,832 (6.88%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 195,562 (28.13) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wanafunzi 451,863 (64.99%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Uchambuzi zaidi wa takwimu za ufaulu unaonesha kuwa wanafunzi 451,863 sawa na asilimia 64.99 walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata kati ya alama 0 na 2.5. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kukosa uelewa kuhusu umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii hivyo kutoa hoja zisizo sahihi. Wanafunzi 204,076 sawa na asilimia 29.4 walishindwa kutoa hoja hata moja, hivyo kupata 0. Katika kundi hili, Baadhi walielezea dhima za fasihi na wengine walibainisha sifa za lugha kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama vile: (a) *Huelimisha jamii*, (b) *Huburudisha jamii*, (c) *Lugha ni sauti ya nasibu yenye kuleta hamasa ili mtu kuweza kuelewa kwa haraka*, (d) *Husaidia pia kuelezwa au kujua kitu kwa kutumia lugha wanajamii hupata hamasa ya kutaka kujua kwa haraka*, na (e) *Kitambulisho cha jamii*. Baadhi ya hoja alizoelezea hususani zilizopo katika vipengele (a), (b), na (e) ni dhima za fasihi, hivyo hazihusiani na hoja zinazoelezea umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii kama vile (a) *Kukuza hadhi ya lugha*, (b) *Kudumisha taratibu za kisarufi za lugha*, (c) *Kusaidia kukamilisha*

*mawasiliano baina ya watu*, (d) *Kuhakikisha uwiano wa maneno*, na (e) *Kuipa lugha mvuto.* Kwa ujumla, wanafunzi hao walionesha kukosa umahiri kuhusu umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii, hivyo kueleza mambo yasiyohusiana na matumizi ya lugha na kupata alama za chini. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali hili.



**6. Kwa kutoa hoja tano, eleza umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii.**

(a) Kukua kwa lugha

(b) Kudumisha lugha

(c) Hakutakuwa na mgogoro wote katika mawasiliano.

(d) Kuwa na amani katika jamii hiyo.

(e) Kukua kwa maendeleo

Kielelezo Na. 6.1: *Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 6*

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyepata alama 0 kwa kutoa hoja zisizo sahihi kuhusu umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii katika vipengele (b), (c), (d), na (e) ambapo alitoa hoja zisizohusiana na swali lililoulizwa.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 195,562 sawa na asilimia 28.13 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa na alama kati ya 3 hadi 6 kutokana na kutoa hoja sahihi 2 au 3 pekee kuelezea umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa hoja sahihi zifuatazo: (a) *Hurahisisha mawasiliano,* (b) *Huipa lugha hadhi yake*, na (d) *huondoa utata katika tungo*. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alishindwa kueleza kwa usahihi umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii kwenye vipengele (c) na (e) kwa kuandika *gharama ndogo* na *hupokea mabadiliko ya papo kwa papo.* Hoja hizi zinaelezea sifa za fasihi simulizi kinyume na matakwa ya swali hili, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi 47,832 sawa na asilimia 6.88 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10 kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa kutumia lugha fasaha, kwa kutoa hoja 4 hadi 5 sahihi na kupata alama za juu. Wanafunzi hao walitoa hoja sahihi zifuatazo: (a) *Hukuza hadhi ya lugha*, (b) *Hudumisha taratibu za kisarufi za lugha*, (c) *Husaidia kukamilisha mawasiliano baina ya watu*, (d) *Huhakikisha uwiano wa maneno*, na (e) *Huipa lugha mvuto.* Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

6. Kwa kutoa hoja tano, eleza umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii.

(a) Huipa lugha mvuto wa urembo - Mtu anapotumia lugha fasaha hutumika maneno vizuri na kuupa lugha mvuto wa urembo.

(b) Huondoa utata katika mawasiliano. Lugha fasaha huweza kuondoa utata katika mawasiliano pale mtu anapotumika maneno kwa ufasaha.

(c) Huhakikisha ukamilika kwa mawasiliano - Lugha fasaha huhakikisha ukamilika kwa mawasiliano kwani wazungumzaji wataelewana.

(d) Huzingatia ~~st~~ sheria au taratibu za Lugha kisarufi. Lugha fasaha huweza kuzingatia sheria zote za lugha kisarufi na kuweza kupata mawasiliano bora.

(e) Hukuza hadhi ya lugha - Lugha fasaha huweza kukuza hadhi ya lugha kwani mtumiaji atakuwa ana zingatia sheria za lugha fasaha


Kielelezo Na. 6.2: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6*

Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyetoa hoja sahihi kuhusu umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii.

### 2.2.5 Swali la 7: Matumizi ya Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuelewa kanuni za msingi za lugha ya mazungumzo. Swali lilimtaka mwanafunzi kuelezea mambo makuu matano yanayotakiwa kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo.

Wanafunzi 695,263 sawa na asilimia 99.99 ya waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu ambapo wanafunzi 170,456 sawa na asilimia 24.52 pekee ndio walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kiasilimia.





**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 50,329 (7.24%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 120,127 (17.28%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wanafunzi 524,807 (75.48%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu wa chini ambapo wanafunzi 524,807 sawa na asilimia 75.48 waliofanya upimaji huu walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata kati ya alama 0 na 2.5. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kukosa umahiri wa matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Miongoni mwao,

wanafunzi 424,014 sawa na asilimia 61.0 walishindwa kabisa kuelezea mambo ya kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi ya wanafunzi walielezea tofauti kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi kama vile *kupokea mabadiliko, matumizi ya ishara mbalimbali* kinyume na matakwa ya swali. Wanafunzi wengine walibainisha sifa za kisarufi kama vile *matamshi, maumbo* na *miundo* ya maneno katika tungo badala ya kuelezea mambo ya kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo kama vile: (a) *Uhusiano baina ya wazungumzaji*; (b) *Mahali pa mazungumzo*; (c) *Wakati wa mazungumzo*; (d) *Lengo la mazungumzo*; na (e) *Mada ya mazungumzo*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili na kupata 0.


7. Eleza mambo makuu matano yanayotakiwa kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo.

(a) Maana ya neno: inatakiwa yulikane maana halisi ya neno husika

(b) muundo: inatakiwa yulikane jinsi neno ulivyo undwa kwa ujanisi wake.

(c) mtindo: inatakiwa yulikane mtindo ulio [illegible] husika kwenye neno

(d) uradidi wa maneno unatakiwa kuzingatiwa

(e) lajudhi ya maneno inatakiwa kuzingatiwa kwani inaweza kupotosha maana ya maneno yatakayo husika.

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7

Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kueleza mambo makuu matano ya kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo kwa kuandika mambo yanayohusu *lugha, matawi ya kisarufi, uundaji wa maneno,* pamoja na vipengele vya fani (*mtindo*) katika uhakiki wa kazi za kifasihi kinyume na matakwa ya swali.

Aidha, wanafunzi 120,127 sawa na asilimia 17.28 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kati ya 3 na 6. Uchambuzi wa majibu yao unaonesha kuwa, wanafunzi hao walikuwa na uelewa usiojitosheleza kuhusu mambo ya kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo, kwani walielezea kwa usahihi baadhi ya hoja na kushindwa kuelezea kwa usahihi hoja zingine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika mambo sahihi ya kuzingatiwa katika kuteua maneno na miundo ya tungo kama vile: (a) *Mazingira*, (b) *Uhusiano baina ya wahusika*, (c) *Mada inayozungumzwa* lakini katika vipengele (d) na (e) alitoa hoja sawa na zilizotangulia na kupata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 50,329 sawa na asilimia 7.24 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10. Wanafunzi hao walionesha kuwa na umahiri wa kutosha wa kuelewa mambo makuu matano ya kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo. Kwa mfano, miongoni mwao asilimia 2.1 walielezea kwa usahihi kama vile: (a) *Uhusiano baina ya wazungumzaji*; (b) *Mahali pa mazungumzo*; (c) *Wakati wa mazungumzo*; (d) *Lengo la mazungumzo*; na (e) *Mada ya mazungumzo* hivyo kupata alama zote 10. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za juu katika swali hili.

**7. Eleza mambo makuu matano yanayotakiwa kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo.**

(a) kuzingatia uhusiano baina ya wahusika mfano tunapozungumza na wazazi na marafiki huwa ni tofauti.

(b) kuzingatia wakati wa mazungumzo. mfano uwapo kuwe sherehe na msibani huni ni tofauti

(c) kuzingatia mada ya mazungumzo. mfano kuhusu ajali za barabarani tunatumia maneno yanayoendana na ajali.

(d) kuzingatia lengo la mazungumzo mfano kama lengo lako ni kuonya au kukanya jamii

(e) kuzingatia mahali au mazingira. mfano tunatumia lugha tofauti tunapokuwepo kanisani na madukani.

Kielelezo Na. 7.2: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7*

Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeelezea kwa usahihi mambo makuu matano ya kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na miundo ya tungo.

### 2.2.6 Swali la 8: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi* hususani mada ndogo ya *Njia za Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima maarifa aliyonayo mwanafunzi ya kuchambua faida na hasara za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi. Swali lilimtaka mwanafunzi kuelezea faida mbili na hasara tatu za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili yaani (a) na (b), ambapo kipengele (a) kilikuwa na vipengele vidogo viwili (i) na (ii) na kipengele (b) kilikuwa na vipengele vitatu (i), (ii) na (iii).

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 695,269 sawa na asilimia 100 ya waliofanya upimaji wa somo hili. Hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu, ambapo asilimia 64.32 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwa asilimia.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi**

| Alama | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 248,057 | 35.68 |
| 3.0 - 6.0 | 290,750 | 41.82 |
| 6.5 - 10 | 156,462 | 22.50 |

Jedwali Na. 2 linaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ambapo asilimia 22.50 walifaulu kwa kiwango kizuri, asilimia 41.82 kiwango cha wastani, na asilimia 35.68 kiwango hafifu.

Aidha, wanafunzi 156,462 sawa na asilimia 22.50 waliojibu swali hili walifanya vizuri na kupata alama za juu kati ya 6.5 hadi 10 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa mada ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*. Wanafunzi hao walieleza kwa usahihi faida

za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi kama vile (a) (i) *Haibadiliki mara kwa mara* na (ii) *Hudumu kwa muda mrefu.* Katika kipengele (b), walieleza hasara tatu za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi kama vile (i) *Hupoteza vionjo,* na (ii) *Hukosa utendaji.* Majibu hayo kwa ujumla yalikidhi matakwa ya swali hili. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali hili na kupata alama zote 10.

8. Eleza faida mbili na hasara tatu za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi.

(a) Faida

(i) Hudumu kwa muda mrefu. Kazi za fasihi simulizi katika maandishi huweza kukaa kwa muda mrefu na kuendelea kutumika na jamii tofauti na Njia nyingine za Uhifadhi.

(ii) Huifikia hadhira katika eneo kubwa. Kazi za fasihi simulizi katika maandishi huweza kusambazwa katika maeneo mbalimbali na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

(b) Hasara

(i) Hubagua kati ya wanaojua kusoma na wasiojua kusoma. Kazi za fasihi simulizi katika maandishi hujumuisha wanaojua kusoma tu. Hivyo wasiojua kusoma hukosa kazi hiyo ya fasihi simulizi.

(ii) Gharama. Kazi za fasihi simulizi katika maandishi huhitaji fedha katika uandaaji wake na usambazaji wake hivyo ni gharama kwa kuwa huweza kutumia kiasi kikubwa cha fedha.


(iii) Fanani na hadhira hawaonani ana kwa ana. Hadhira hukosa nafasi ya kuuliza maswali mahali asipoelewa.

Kielelezo Na. 8.1: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8*

Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeelezea kwa usahihi faida mbili na hasara tatu za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi 290,750 sawa na asilimia 41.82 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani. Baadhi ya wanafunzi hao walielezea faida pekee na kushindwa kuelezea hasara za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi au kinyume chake. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alielezea kwa usahihi hasara tatu na kushindwa kueleza faida mbili za kuhifadhi kazi za fasihi katika maandishi. Hali kadhalika, wanafunzi wengine walitoa hoja zisizojitosheleza kuhusu faida au hasara za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi hivyo kupata alama za wastani. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa umahiri wa njia za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi.

Hata hivyo, wanafunzi 248,057 sawa na asilimia 35.68 ya waliofanya upimaji walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata kati ya alama 0 na 2.5. Wanafunzi hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi*; hivyo kushindwa kuelezea faida na hasara za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi ya wanafunzi walitaja njia mbalimbali za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kama vile tepurekoda, vinasasauti na filamu. Wengine walielezea faida au hasara chache za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi, hivyo kupata alama za chini na kuwa na ufaulu hafifu. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alielezea mambo yasiyohusiana na faida au hasara za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi katika maandishi kama vile: (a) (i) *Fasihi simulizi huifadhiwa kichwani* na (b) (i) *Huifadhiwa kwa njia ya maandishi*; na (a) (ii) *Fasihi simulizi ni kongwe* na (b) (ii) *Fasihi andishi si kongwe*. Wanafunzi hao walitakiwa kuelezea faida na hasara za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi kama vile (i) *Haibadiliki mara kwa mara* na (ii) *Hudumu kwa muda mrefu* (faida) na (i) *Hupoteza vionjo,* (ii) *Hukosa utendaji*, na (iii) Fanani haonekani (hasara). Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyefanya vibaya swali hili na kupata 0.



8. Eleza faida mbili na hasara tatu za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi.

(a) Faida

(i) Haina gharama

(ii) Ni mali ya jamii nzima.

(b) Hasara

(i) Inapotea kadri unavyozidi kuzeeka kwasababu hufadhiwa kwenzia ya kichwa.

(ii) Fasihi simulizi inatumika na watu wote wasomi pia na wasio wasomi.

(iii) Fasihi simulizi hupotea kwa haraka.


Kielelezo Na. 8.2: *Sampuli ya majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 8*

Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeelezea sifa za fasihi simulizi badala kuelezea faida na hasara za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika maandishi.

### 2.2.7 Swali la 9: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu dhana ya wahusika katika kazi za fasihi. Swali hili lilimtaka mwanafunzi kuelezea kwa hoja tano umuhimu wa wahusika katika kazi za fasihi.

Wanafunzi 695,267 sawa na asilimia 99.99 waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha chini zaidi cha ufaulu ikilinganishwa na maswali yote yaliyopimwa, ambapo wanafunzi 111,778 sawa na asilimia 16.08 pekee walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 8:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 9*

Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 14,848 (2.14%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 6.5 hadi 10, wanafunzi 96,930 (13.94%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 na wanafunzi 583,489 (83.92%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 2.5.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa, wanafunzi 583,489 sawa na asilimia 83.92 ya waliofanya upimaji walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata kati ya alama 0 na 2.5. Wanafunzi hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi.* Hivyo, wanafunzi hao walishidwa kuelezea umuhimu wa wahusika katika kazi ya fasihi kama vile *kuibua dhamira*, (b) *kufikisha ujumbe uliokusudiwa*, (c) *kuibua migogoro*, (d) *kuonesha uhalisia wa maisha*, na (e) *kuonesha utendaji*. Kutokana na kukosa umahiri huo, baadhi ya wanafunzi hao walitaja vipengele mbalimbali vya fani katika kazi za fasihi kama vile: *matumizi ya lugha, muundo, mtindo, mandhari* na *wahusika*. Wanafunzi wengine walitoa hoja zinazohusu dhima za fasihi kama vile *kuelimisha*, (b) *kuburudisha*, (c) *kukosoa*, (d) *kuadabisha*, na (e) *kutunza historia ya jamiii* badala kuelezea umuhimu wa wahusika katika kazi ya fasihi kama swali lilivyotaka. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili.

9. Kwa kutoa hoja tano, eleza umuhimu wa wahusika katika kazi ya fasihi.

(a) Wanyama, hii inamaanisha ya kuwa katika fasihi huwa kunavitu mbalimbali ambavyo inawakilisha fasihi maja wapo wanyama

(b) Binadamu, hii inamaanisha yakuwa katika fasihi huwa na wahusika mbalimbali katika fasihi ambao huwa na msimamo na pia kuelimisha jamii hata kuadabisha.

(c) huleta maana iliyo kamili, hii inamaanisha ya kuwa fasihi huwa inaleta maana iliyo kamili ili kufikisha ujumbe kwa jamii iliyo kusudiwa

(d) Huadabisha, hii inamaanisha ya kuwa fasihi huadabisha watu mfano mtoto alikuwa na tabia mbaya baada kusikiliza stori akapata funzo.

(e) Inaleta maana kimsingi, hii inamaanisha ya kuwa wahusika katika fasihi huleta maana katika jamii

Kielelezo Na. 9.1: *Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 9.*

Katika kielelezo Na. 9.1, mwanafunzi alielezea baadhi ya *aina za wahusika*, *dhima za lugha* na majibu mengine mseto yasiyohusiana na kiini cha swali hili, hivyo kupata alama hafifu.

Vilevile, uchambuzi wa kina unaonesha kuwa wanafunzi 96,930 sawa na asilimia 13.94 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kati ya 3 na 6. Ufaulu huu ulitokana na wanafunzi hao kuwa na uelewa usiojitosheleza kuhusu wahusika kama kipengele muhimu cha uhakiki wa kazi za fasihi. Hali hii iliwafanya kutoa hoja zisizojitosheleza kuhusu umuhimu wa wahusika katika kazi za fasihi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa hoja sahihi kama vile (a) *Huweza kuwakilisha dhana*, (b) *Huweza kuibua hisia za hadhira*, na (d) *Huweza kufikisha ujumbe wa msanii kwa hadhira*. Hata hivyo, mwanafunzi huyo alishindwa kuelezea kwa usahihi vipengele (c) na (e) kwa kuandika *huweza kuonesha uhusiano kati ya vitu na mazingira* na h*uweza kuvuta taswira ya jambo fulani*, majibu yasiyo sahihi hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 14,848 sawa na asilimia 2.14 waliojibu swali hili walifanya vizuri na kupata alama za juu kati ya 6.5 na 10 kutokana na kuwa na umahiri wa kutosha kuhusu umuhimu wa wahusika katika kazi za fasihi. Wanafunzi hao walitoa hoja sahihi tano kuelezea umuhimu wa wahusika katika kazi ya fasihi kama vile: (a) *Kuibua dhamira*, (b) *Kufikisha ujumbe uliokusudiwa*, (c) *Kuibua migogoro*, (d) *Kuonesha uhalisia wa maisha*, na (e) *Kuonesha utendaji*. Wanafunzi hao pia walitoa ufafanuzi mzuri uliokidhi matakwa ya swali katika hoja zote tano. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi swali hili na kupata alama zote 10.

9. Kwa kutoa hoja tano, eleza umuhimu wa wahusika katika kazi ya fasihi.

(a) Husaidia kuonyesha uhalisia wa jambo linalowasilishwa. Wahusika husaidia kuonyesha uhusiano uliopo kati ya dhana inayozungumziwa na hali halisi iliyopo katika jamii.

(b) Huifanya kazi ya fasihi kuwa na mvuto; mfano wahusika kama wanyama au mizimu na vitu visivyo -hai huipamba kazi ya fasihi pale wanapotumika kuwasilisha kazi ya fasihi

(c) Huchangamsha hadhira husika; Hadhira huweza kuburudika na pia kuwachangamsha hivyo kuwatoa uchovu na kuongeza umakini.

(d) Husaidia kuonyesha matendo yaliyodhahiri au yenye; kufikirika. Mfano katika fasihi simulizi wahusika huo -nyesha matendo dhahiri mfano uimbaji, usimulizi na kadhalika.

(e) Huifanya fasihi kuwa hai; Ili fasihi iwe hai ni pamoja na uwepo wa wahusika, kushirikisha hadhira mfano kupiga makofi pia kuwa na matendo yaliyodhahiri au yakufikika.

Kielelezo Na. 9.2: *Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 9*

Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeelezea kwa usahihi hoja zote tano kuhusu umuhimu wa wahusika katika kazi za fasihi.


## 2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lililomtaka mwanafunzi kuandika barua rasmi. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 15.

### 2.3.1 Swali la 10: Uandishi wa Barua

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi* hususani mada ndogo ya *Uandishi wa Barua Rasmi* na lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi wa uandishi wa barua rasmi. Swali lilimtaka mwanafunzi kuandika barua kwa mkuu wa shule yenye lengo la kuomba ruhusa ya kwenda kwenye matibabu katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma.

Wanafunzi 695,247 sawa na asilimia 99.99 ya waliofanya upimaji huu walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo asilimia 91.96 walifaulu kwa kiwango kizuri hadi cha wastani. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kiasilimia.




**Chati Na. 9:** *Asilimia ya Ufaulu wa Wanafunzi katika Swali la 10*

Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili kiasilimia, ambapo wanafunzi 387,461 (55.73%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 10 hadi 15, wanafunzi 251,888 (36.23%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 na wanafunzi 55,898 (8.04%) walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata 0 hadi 4.

Uchambuzi wa kina unaonesha kuwa wanafunzi 387,461 sawa na asilimia 55.73 walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata alama kati ya 10 na 15 kutokana na kuwa na umahiri wa kutosha wa uandishi wa barua rasmi. Ufaulu mzuri katika swali hili unaonesha kuwa, wanafunzi wengi walikuwa na umahiri wa kutosha wa mada ya *Uandishi wa barua rasmi.* Wanafunzi hao waliandika barua kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uandishi wa barua rasmi kama vile *anuani ya mwandishi* inayoandikwa upande wa kulia; *tarehe* chini ya anuani ya mwandishi; *anuani ya mwandikiwa* iandikwayo chini ya tarehe upande wa kushoto; *mwanzo wa barua*; *kichwa cha barua; barua yenyewe*; *mwisho wa barua*; *saini ya mwandishi*; *jina la mwandishi*; na *cheo cha mwandishi*. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika kwa usahihi barua rasmi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uandishi wa barua rasmi na kupata alama za juu. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili kwa kukidhi matakwa ya swali.

**10 Umepata matatizo ya kiafya hivyo unahitaji kwenda kutibiwa hospitali ya Mkoa wa Dodoma. Andika barua kwa Mkuu wa Shule kuomba ruhusa ya siku mbili. Jina lako liwe Juhudi Sabuni na anuani iwe Shule ya Sekondari Tegemeo, S.L.P 130, Dodoma.**

SHULE YA SEKONDARI TEGEMEO,
S.L.P 130,
DODOMA.
30.10.2023.

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI TEGEMEO,
S.L.P 130,
DODOMA.

Ndugu,

YAH; KUOMBA RUHUSA KWA AJILI YA KWENDA KUTIBIWA

Husika na kichwa cha barua hapo juu.
Mimi ni mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule yako, shule ya sekondari Tegemeo.
Dhumuni au lengo la barua hii ni kuomba ruhusa ya siku mbili kwa ajili ya kwenda kutibiwa katika hospitali ya mkoa Dodoma.
Ni matumaini yangu kuwa ombi langu litajibiwa.

Wako katika ujenzi wa taifa
J. Sabuni
Juhudi Sabuni
Mwanafunzi

Kielelezo Na. 10: *Sampuli ya Jibu Sahihi katika Swali la 10.*

Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi kwa kuzingatia taratibu na kanuni zote za uandishi wa barua.

Aidha, wanafunzi 251,888 sawa na asilimia 36.23 ya waliofanya upimaji huu walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kati ya 4.5 na 9.5 kutokana na kukidhi baadhi ya matakwa ya swali na kushindwa kukidhi mengine. Baadhi yao waliandika barua yenye anuani ya mwandishi na mwandikiwa lakini kiini cha barua hakikujitosheleza ili kukidhi matakwa ya swali. Pia, wapo ambao hawakuandika jina la mwandishi mwishoni mwa barua. Wanafunzi wengine hawakuandika tarehe, mwanzo wa barua, saini mwishoni mwa barua na cheo cha mwandishi hivyo kupata alama za wastani.

Vilevile, wanafunzi 55,898 sawa na asilimia 8.04 ya waliofanya upimaji huu walifaulu kwa kiwango hafifu kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya uandishi wa barua rasmi. Miongoni mwao walichanganya taratibu na kanuni za uandishi wa barua za kirafiki na rasmi, hivyo kuandika barua ya kirafiki badala ya barua rasmi kama swali lilivyotaka, hivyo kupata alama 0. Wengine walikosa kabisa umahiri wa uandishi wa barua na badala yake waliandika insha kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alinakili maelezo yaliyopo kwenye swali aliloulizwa na kuandika maelezo kuhusu matibabu anayoyataka katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma. Mwanafunzi mwingine aliandika barua yenye muundo wa barua za kirafiki ambayo haikuwa na anuani ya mwandikiwa, mwanzo wa barua, kichwa cha barua, kiini cha barua, mwisho wa barua, saini, jina la mwandishi na cheo cha mwandishi. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika barua isiyokidhi matakwa ya swali.

10 Umepata matatizo ya kiafya hivyo unahitaji kwenda kutibiwa hospitali ya Mkoa wa Dodoma. Andika barua kwa Mkuu wa Shule kuomba ruhusa ya siku mbili. Jina lako liwe Juhudi Sabuni na anuani iwe Shule ya Sekondari Tegemeo, S.L.P 130, Dodoma.

Mimi naitwa juhudi sabuni
natokea shule ya Sekadari Tegemeo
naomba ruhusa niede hospitari ya
ya mkoa kwenye matibabu yangu.

S.L.P 130
NZEGA TABORA

Kielelezo Na. 10.2: *Sampuli ya Jibu Lisilo Sahihi katika Swali la 10*

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeandika maelezo yasiyoendana na barua rasmi na isiyokuwa na muundo wa barua rasmi. Pia, aliandika jina lake **Juhudi Sabuni** kwa kuanza na herufi ndogo hivyo kukiuka kanuni ya uandishi wa majina ya watu.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika mada tano (5) zilizopimwa katika somo la Kiswahili unaonesha kuwa mada mbili zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada ya *Uandishi wa Insha/Utungaji* ilikuwa na kiwango kizuri zaidi cha ufaulu kwa asilimia 91.96 ikifuatiwa na mada ya *Ufahamu* iliyokuwa na ufaulu wa asilimia 70.52. Aidha, mada tatu zilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu zikihusisha mada za *Sarufi* (61.93%), *Fasihi kwa Ujumla* (47.69%) na *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* (29.76%).

Wastani wa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika mada zote kwa mwaka 2023 ni asilimia 60.38, kiwango ambacho ni cha chini kwa asilimia 13.59 ikilinganishwa na mwaka 2022, ambapo wastani wa kiwango cha ufaulu kwa mada kilikuwa asilimia 73.97. Upungufu mkubwa wa ufaulu kwa mwaka 2023 unathibitisha kuwa baadhi ya wanafunzi hawakuwa na umahiri katika mada mbalimbali zilizopimwa kwa mwaka 2023, hivyo idadi kubwa ya wanafunzi walitoa majibu yasiyo sahihi katika maswali mengi.

Mada ya *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* ilikuwa na wastani wa chini zaidi wa ufaulu wa asilimia 29.76 kwa mwaka 2023 ikiwa na upungufu mkubwa wa asilimia 21.76 ikilinganishwa na mwaka2022. Hali hii inaonesha kuwa kuna haja ya kuongeza jitihada zaidi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wake. Hii inatokana na wanafunzi wengi kukosa umahiri katika kufafanua hatua stahiki za kuzingatia ili kupata maana ya neno katika kamusi. Aidha, wanafunzi wengine walishindwa kuelezea umuhimu wa kutumia lugha fasaha katika jamii. Kwa ujumla, mada hii inatakiwa kutiliwa mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri wa maarifa na kuwafanya kuwa mahiri katika matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Ufaulu wa wanafunzi katika mada mbalimbali kwa mwaka 2023 umeainishwa katika **Kiambatisho cha Pekee**.

## 4.0 HITIMISHO

Upimaji wa Kidato cha Pili kwa Mwaka 2023 katika somo la Kiswahili ulizingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili na maswali yote yalipimwa kwa kuzingatia nyanja za utambuzi ambazo ni *kuelewa, kukumbuka, kutumia, kuchambua*, *kutathmini* na *kuunda*. Kwa ujumla, ufaulu wa wanafunzi katika upimaji huu ulikuwa mzuri kwani asilimia 95.19 walifaulu.

Takwimu za ufaulu katika upimaji huu kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022 zinaonesha kuwa, mada ya *Uandishi wa Insha/Utungaji* (91.96%) na *Ufahamu* (70.72%) zimeendelea kuwa na viwango vizuri vya ufaulu, jambo linalodhihirisha kuwa wanafunzi wanao umahiri wa kutosha katika mada hizo. Aidha, mada za *Sarufi* (61.93%) na *Fasihi kwa Ujumla* (47.69%) zimeshuka kutoka kiwango kizuri hadi kiwango cha wastani cha ufaulu. Hata hivyo, mada ya *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* (29.76%) imekuwa na kiwango cha chini zaidi cha ufaulu ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 51.52. Kwa ujumla, uchambuzi umebaini kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi unahitaji kutiliwa mkazo katika mada mbalimbali, kwani kumekuwa na kushuka kwa viwango vya ufaulu katika mada nyingi ikilinganishwa na mwaka 2022.

Uchambuzi umeonesha changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika upimaji huu, kama vile baadhi ya wanafunzi kutokuwa na uelewa wa kutosha wa mada mbalimbali zilizopimwa hususani mada za *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha*, *Fasihi kwa Ujumla*, na *Sarufi.* Aidha, kuna wanafunzi walioonesha kutozingatia ipasavyo matakwa ya maswali, hivyo kuwa na ufaulu hafifu au usioridhisha. Ili kuinua kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika somo la Kiswahili, changamoto hizi zinaweza kutatuliwa kwa kuwapa wanafunzi mazoezi ya kutosha na ya mara kwa mara kuhusu matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali; kuweka msisitizo katika uhakiki wa kazi za kifasihi kupitia vipengele vya fani na maudhui; na matumizi sahihi ya kamusi. Vilevile, wanafunzi wapatiwe mazoezi ya kutosha katika mada za *Mawasiliano* na *Matumizi ya Lugha* ili kuwajengea umahiri na kuimarisha ufaulu.

Kwa upande mwingine, uchambuzi wa ufaulu wa wanafunzi katika maswali yaliyopimwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa, zipo jitihada kubwa zilizofanywa na zinazoendelea kufanywa na wadau mbalimbali wa elimu ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama ilivyodhihirishwa na ufaulu wa jumla wa wanafunzi kwa mwaka 2023 ambapo wanafunzi 660,969 sawa asilimia 95.19 walifaulu.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa wa Kidato cha Pili Mwaka 2023 inatarajiwa itumike ipasavyo ili kuwa chachu na dira ya mabadiliko kutoka viwango vya wastani vya ufaulu na kuwa viwango vizuri vya ufaulu katika mada mbalimbali. Aidha, taarifa hii itawawezesha walimu, wanafunzi, na wadau wengine kuelewa changamoto mbalimbali zinazowakabili katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na kubuni mbinu/mikakati ya kuzitatua ili kuinua kiwango cha ufaulu katika upimaji ujao.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika mada za *Sarufi, Fasihi*, na *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* zilizoonekana kuwa na ufaulu wa wastani ikilinganishwa na mada zingine, walimu wanashauriwa:

(a) kutumia vielelezo vya kufundishia vinavyoakisi matumizi mbalimbali ya sarufi katika lugha ya Kiswahili;

(b) kuongoza wanafunzi katika kufanya utafiti/kazi mradi ili kubaini maana za tanzu mbalimbali za fasihi simulizi;

(c) kutumia mbinu ya *igizo-dhima* ili kuwaongezea wanafunzi ujuzi na maarifa ili kubaini faida/hasara za kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi na kuelezea umuhimu wa wahusika katika kazi za fasihi;

(d) kutumia njia ya majadiliano na vielelezo vya kufundishia (zana za kufundishia) zinazopatikana katika mazingira halisi;

(e) Mada ya *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* zifundishwe kwa vitendo ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi kwa kulinganisha kinachofundishwa na matumizi halisi ya lugha katika jamii; na

(f) kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote katika muhtasari wa somo la Kiswahili ili kuchochea udadisi miongoni mwa wanafunzi.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

**Uchambuzi wa Viwango vya Ufaulu wa Wanafunzi katika Mada kwa Mwaka 2023**

| Na. | Mada | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya Swali | % ya ufaulu (alama 30$^+$) | | |
| 1. | *Uandishi wa Insha/Utungaji* | 1 | 91.96 | 91.96 | Vizuri |
| 2. | *Ufahamu* | 1 | 70.52 | 70.52 | Vizuri |
| 3. | *Sarufi* | 4 | 96.67 | 61.93 | Wastani |
| | | 5 | 27.19 | | |
| 4. | *Fasihi kwa Ujumla* | 2 | 62.67 | 47.69 | Wastani |
| | | 8 | 64.32 | | |
| | | 9 | 16.08 | | |
| 5. | *Mawasiliano na Matumizi ya Lugha* | 6 | 35.01 | 29.76 | Wastani |
| | | 7 | 24.52 | | |

